

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Barua zote zianjikwe na kutumwa kwa:

Simu: +255 659 566703 (Direct line)

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P. 70, SIKONGE
TABORA

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

TAREHE: 04/11/2021

TANGAZO
LA
KUTOA HUDUMA YA USAFI KWENYE OFISI ZA
HALMASHAURI
LGA/121/2021/2022/NC/02

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inapenda kuwatangazia wananchi wote wenye Vikundi au Makampuni yenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya Usafi katika Ofisi za Halmashauri na maeneo mbalimbali yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kazi hii ni kuanzia tarehe 01 Desemba, 2021 hadi tarehe 30 Juni, 2022.
2. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.
3. Vitabu vya Kotesheni vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 30,000/ kwa Vikundi au Kampuni itakayomba kazi hii
4. Kotesheni zote ziwe na nakala halisi (original moja) na nakala (copy) mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa;

"KOTESHENI NA. LGA/121/2021 - 2022 /NC/02" KWA UTOAJI WA HUDUMA YA USAFI KATIKA OFISI NA MAENEO MBALI MBALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

5. Maombi yote yapelekwe (yatumwe) kwa *Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, S.L.P 70, SIKONGE.*
6. Kikundi au Kampuni iwe na Leseni halali ya Biashara na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
7. Kikundi au Kampuni ionyeshe utambulisho kwamba inalipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
8. Kikundi au Kampuni iwe imesajiliwa na Msajili wa Makampuni na kivuli cha usajili kiambatanishwe kwenye maombi yake
9. Kikundi au Kampuni ionyeshe uzoefu wa Kazi husika
10. Kikundi au Kampuni ionyeshe kiasi cha fedha atakacholipwa na Halmashauri kwa kila Mwezi.
11. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni *siku ya Alhamisi tarehe 18.11.2021 saa 4:00 Asubuhi.* Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya waombaji au wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
12. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.



Seleman Pandawe

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SIKONGE**

**MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE.**